



## Waelezeni watu yale wanayoyafahamu, Hivi mnataka akadhibishwe (apingwe) Mwenyezi Mungu na Mtume wake

Kutoka kwa Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Amesema: "Waelezeni watu yale wanayoyafahamu, Hivi mnataka akadhibishwe (apingwe) Mwenyezi Mungu na Mtume wake?".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Anaelekeza Kiongozi wa waumini Ally bin Abii Twalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kuwa haitakiwa watu wote kuelezwa isipokuwa yale mambo ambayo ni maarufu tena yenye kuwanufaisha watu katika msingi wa dini yake na hukumu yake miongoni mwa tauhidi na kuwabainishia watu halali na haramu, na kuacha yenye kupoteza lengo hilo; katika yale yasiyokuwa na haja ndani yake, au yakawa ni katika mambo ambayo ni sababu ya kupingwa ukweli na kutokubalika kwake katika yale ambayo wanatatizika kuyafahamu, na inakuwa kwao vigumu kuyajua.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3344>

